# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO

### ARUSHA VTC

### 2024

Simu: 0736500507 P. O. BOX 509, ARUSHA

Nukushi: arushavto@veta.go.tz

www.veta.go.tz

Kumb| Na; 4/1/2024

---

Ndugu

..............................................................................

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA ARUSHA VTC Mwaka 2024

MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika

   Fani ya ....................................

   Katika ngazi Level One

   mwaka wa I ..............................
2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili - mitatu (2-3)
3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 15/01/2024
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa
6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni
9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii
10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa. Fedha ikishalipwa hairudishwi. Kama fedha za tahadhali (caution Money) hazikutumika zitarudishwa
11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo

______________________________

B.D MREFU

MKUU WA CHUO

MAELEZO MUHIMU.

1. **Mwanzo wa Muhula 2024.** Mafunzo *Yataanza* Jumatatu tarehe **15January, 2024**. Nafasi yako atapewa Mtanzania mwingine ukishindwa kufika Chuoni **kipindi cha wiki mbili (2) kuanzia tarehe ya kufungua chuo.** Unatakiwa kufika chuoni sio zaidi ya saa 10:00 Alasiri.
2. **Muda wa Mafunzo.** Mafunzo yamepangiliwa kwa hatua tatu. Hatua ya Kwanza (Level I), Hatua ya Pili (Level II) na Hatua ya Tatu na ya mwisho (Level III).
3. **Sifa zako.** Unatakiwa kuja na cheti halisi cha Darasa la Saba/Kidato cha nne (original academic certificate/result slip) na nakala yake (photo copy). Baada ya cheti kuthibitishwa na Msajili/Dawati la Kujiandikisha, utaruhusiwa kuondoka na cheti chako halisi na nakala kubaki Chuoni kwa kumbukumbu. Kumbuka: Living Certificate/Copy havikubaliki.
4. **Usalama**. Unatakiwa kujinunulia "Safety Boots" yenye sifa zifuatazo: - steel toe cap; oil resistant sole. (*Wanafunzi wa Ushonaji nguo hawahusiki*). Ikiwa huna uhakika na Maelekezo yoyote hapa, fika Chuoni Ofisi ya Msajili kwa Ufafanuzi.
5. **Mahitaji Maalum** Unatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako binafsi Ukiwa Chuoni. Kila mwanafunzi anaelekezwa kuzingatia na kutekeleza maelekezo hayahapa.
    a. Mashati mawili meupe (mikono mifupi) ya tetroni.
    b. Suruali 2pc rangi ya blue **– zinapatikana chuoni**.
    c. Jozi moja ya viatu vyeusi vya ngozi
    d. Vifaa vya hesabu (mathematical set) Kalamu na penseli
    e. Daftari 8 aina ya counter book 4 quire.
    f. Sweta moja ya bluu, mavazi ya heshima na vifaa vya usafi binafsi.
    g. Ovaroli/Ovakoti – rangi ya blue **yanapatikana chuoni**
    h. Bima ya afya NHIF **NI LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI**
    i. Godoro kwa wanafunzi wa bweni (kipimo mita 2.5)
    j. Photocopy paper (ream1)
    k. Fyekeo/PANGA, MFAGIO MGUMU(HARD BROOM), RUBBER SQUIZER.
    l. Blanketi, Mashuka 2 rangi ya blue, Neti ya mbu, Sahani, Ndoo ya kuogea/kufulia,Kikombe na Kijiko.

6. **Ada.** Ada ya Bweni na kutwa kwa mwaka inajumuisha pia gharama ya vitu vilivyoorodheshwa kwenye jedwali hapa chini. tafadhali zingatia maelekezo unayopewa katika ulipaji wa ada yako.
7. **SHERIA ZA CHUO.** Chuo cha **VETA Arusha** kinazo Sheria na Kanuni kwa Mujibu na Muongozo Uliotolewa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania (VETA) Nakala imeambatanishwa na barua ya wito.

**JEDWALI LA KWANZA; MALIPO YA ADA NA GHARAMA NYINGINE KWA MUHULA KWANZA 2024**

| | MUHULA WA KWANZA 2024 | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **MAHITAJI** | **KUTWA** | **BWENI** | **MAELEKEZO** |
| 1 | ADA YA MAFUNZO | 30,000.00 | 60,000.00 | PATA CONTROL NUMBER |
| 2 | NEMBO YA VETA 1PC | 5,000.00 | 5,000.00 | LIPA KWENYE CONTROL NUMBER UTAKAYOPEWA NA CHUO |
| 3 | TAHADHARI | 20,000.00 | 20,000.00 | |
| 4 | KITAMBULISHO | 5,000.00 | 5,000.00 | |
| 5 | MICHEZO | 10,000.00 | 10,000.00 | |
| 6 | MAHAFALI | 25,000.00 | 25,000.00 | |
| | **JUMLA KUU** | **95,000.00** | **125,000.00** | |

**JEDWALI LA PILI; GHARAMA ZA MAHITAJI YAFUATAYO ZINAPATIKANA CHUONI HIVYO MZAZI AJE NA FEDHA TASLIMU SIKU YA KURIPOTI CHUONI.**

| | **MAHITAJI** | **IDADI** | **GHARAMA YA JUMLA** |
|---|---|---|---|
| 1 | T-SHIRT | **1** | 15,000.00 |
| 2 | OVER COAT ( USHONAJI TU) | **1** | 30,000.00 |
| 3 | OVERALL | **1** | 35,000.00 |
| 4 | SURUALI | **2** | 50,000.00 |
| 5 | BIMA YA AFYA NHIF | **1** | 50,400.00 |
| | **JUMLA KUU** | | **180,400.00** |

8. UTARATIBU WA MALIPO

Ada italipwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itafanyika Januari 2024. Nusu ya Ada Unapoingia na Nusu iliyobakia Muhula wa Pili Julai 2024 kwa Bweni au Kutwa

Gharama kwa mahitaji mengine zitalipwa kwenye control namba utakayopewa na Mhasibu wa chuo.

NAMNA YA KULIPA ADA.

**Mwanafunzi afike Chuoni VETA Arusha na atapewa namba ya malipo ya serikali (control number) ya kulipia ADA**

9. **ADA ZA MTIHANI.** Watakaofanya vizuri katika mafunzo na kufikia viwango/sifa za ufaulu, wataruhusiwa kufanya Mtihani wa Taifa “Competence Based Assessment” [CBA] na watapaswa kulipia ada ya mtihani huo. Wazazi/Walezi wataarifiwa Kiasi cha ada wakati wa likizo ndefu, mwezi June/July 2024.

10. **BIMA YA AFYA.** Kila Mwanafunzi Anatakiwa kuwa na Bima ya Afya ya NHIF. Endapo anayo Bima ya nyumbani Aje nayo hata hivyo; ***Mwanafunzi hatapokelewa chuoni bila kuwa na bima ya Afya***.

11. **KUPOKELEWA.** Waliolipa ada kamili, Kuwa na vifaa vilivyotajwa na kutimiza masharti yote yaliyoandikwa hapo juu, Ndio Watapokelewa Chuoni. Utatakiwa kuonyesha vitu hivi Kwa walimu wa Dawati la kusajiliwa Chuoni Utakaporipoti na Utapewa Kibali cha Usajili Ili kupokelewa katika Fani yako na Bwenini.

**Nakutakia Mafunzo Mema Na Karibu Sana VETA ARUSHA.**

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

To Medical Officer (Government Hospital)

……………….....................………..……………….

…………………………………..........................……

…………………………………....................………..

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine the above named candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as………………………………………………………………………………………

i) Eye sight…………………………………………………………………………….........

ii) Hearing ……………………………………………………………………………..........…

iii) Asthma…………………………………………………………………………..........….

iv) Other serious disease…………………………………………………………….............

## MEDICAL CERTIFICATE:

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Date……………Designation…………………………..Signature & Official stamp…………………………

KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

a) MWANACHUO

Mimi ……………………………………………………ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa na nina ahidi kuzingatia sheria na kanuni za Chuo.

Sahihi……………………………………………….Tarehe………………………………………………………

b) MDHAMINI:

Mimi……………………………………………….S.L.P……………………Wilaya/Mkoa……………………
Ninathibitisha kuwa ninamdhamini aliyetajwa hapo juu na nitamlipia ghrarama zote za mafunzo (ada) n.k. pamoja na nauli wakati wote wa kwenda Chuoni na kurudi nyumbani kwa likizo na baada mafunzo.

Tarehe……………………………………Sahihi……………………………………………

Nambari za Simu.........................................................................................